# SAWA WANAWAKE TANZANIA (SAWA)

## Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009





## SOTE TUNAWAJIBU WA KUMLINDA MTOTO



# Sheria

© Sawa Wanawake Tanzania, June 2023

a mtoto

# Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009



## Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009

Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 ni waraka unaoshughulikia masuala mengi ya kitaifa yanayohusu haki na ulinzi wa mtoto. Sheria hii pia imechukua mikataba na makubaliano mbalimbali ya kimataifa yanayohusu haki za mtoto, na vilevile kutoka kwenye sera ya taifa ya watoto. Inaweka bayana muundo unaolenga kumpa mtoto kinga pamoja na viwango kwa ajili ya utoaji haki kwa watoto. Vipengele vilivyomo kwa ajili ya watoto wanaohitaji matunzo nje ya makazi yao, na vilevile kanuni za kudhibiti ajira za watoto zimepewa nguvu zaidi katika sheria hii mpya Na. 21 ya mwaka 2009

# Ifahamu sheria ya Mtoto

Sheria hii imelenga kuimarisha ulinzi, matunzo na haki za watoto Tanzania Bara. Sheria hii imeainisha haki ya mtoto kulelewa na Wazazi, haki ya kupewa jina kuwa na utaifa, haki ya kupata mahitaji ya msingi kama chakula, malazi, mavazi, matibabu, chanjo, elimu, pamoja na haki ya kucheza na kuburudika.




Ni kinyume na sheria kufanya vitendo vya Ubaguzi, unyanyasaji na ukatili dhidi ya watoto. Sheria hii pia imeweka mfumo utakaohakikisha kuwa watoto wanapata haki zao za kisheria aidha wawe wamekinzana na sheria, wameingia kwenye mfumo wa sheria au wameshuhudia vitendo ambavyo wanajikuta wameingia kwenye mfumo wa sheria kama mashuhuda wa vitendo vya jinai,mirathi na kadhalika.



# Wajibu wa wazazi na walezi katika kuhakikisha watoto wanapata haki zao za msingi

• Wazazi na walezi wana wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba watoto wanapelekwa kwenye chanjo, wanapatiwa huduma za afya, wanaandikishwa na kwenda shule, wanafuatiliwa maendeleo yao shuleni, wanasikilizwa na kupewa miongozo na matunzo.

• Jamii inatakiwa iwe bega kwa bega katika kufanikisha wajibu huu kwa kuhakikisha haki za mtoto zinalindwa na kuchukua hatua pale ambapo watoto wanaonekana kunyimwa haki zao.

• Wazazi, walezi na jamii wana wajibu wa kuhakikisha kwamba watoto wote, wakiwemo wale walio katika mkinzano na sheria wanafurahia haki zao na kutekeleza wajibu wao kikamilifu.

• Wazazi, walezi na jamii wana wajibu wa kuhakikisha kwamba wanawaongoza watoto katika kutekeleza wajibu wao kikamilifu.

## Ajira na watoto

Watoto wana ruhusa ya kufanya kazi baada ya kutimiza umri wa miaka 14. Kazi haipaswi kumzuia mtoto kuhudhuria masomo au kupata muda wa kujisomea na kupumzika. Watoto wasiajiriwe kufanya kazi nyakati za usiku. Yeyote anayewafanyisha kazi watoto kupita kiasi, au asiyewalipa ujira unaostahili, basi anavunja sheria hii.



**Kazi ya hatari: maana yake ni kazi yoyote inayomfanya mtoto awe katika hatari ya kuumia kimwili au kiakili. Kwa mfano, kazi kwenye machimbo au kazi ya kupigana vita**



## MAHITAJI YA MSINGI KWA UKUZI WA MTOTO

chakula, mavazi na mahali salama pa kuishi ni haki ya msingi kwa watoto. Wazazi na walezi hawana budi kuwalinda watoto dhidi ya madhara yoyote.



## AFYA YA MTOTO

Inapotokea watoto kuugua, basi wapelekwe hospitalini. Wazazi hawana budi kuhakikisha kwamba watoto wanapata  kinga dhidi ya magonjwa mbalimbali.



## ELIMU KWANZA

Wazazi hawana budi kuwapeleka watoto shuleni na kuwapa nafasi ya kucheza na kupumzika. Matunzo na huduma maalumu zitolewe kwa watoto wanaoishi na ulemavu ili nao waweze kuhudhuria  shule kama watoto wengine.Watoto wote wana haki ya kupata elimu ya msingi ambayo ni rasmi. Hii inalenga kumpatia maarifa ya msingi na muhimu.

## Haki ya Kutoa Maoni





Mtoto ana haki ya kushirikishwa na kutoa maoni. Hakuna mtu anayeruhusiwa kumnyima mtoto mwenye uwezo wa kutoa maoni haki ya kueleza maoni, kusikilizwa na kushiriki katika kufanya maamuzi yatakayoathiri ustawi wake.





# Jukumu la ulinzi wa mtoto

Ulinzi na usalama wa mtoto sio jukumu la maafisa wa ustawi wa jamii peke yao ni jukumu la Taifa kwa ujumla. Hakuna anayeruhusiwa kumdhuru, kumwumiza au kumnyonya mtoto. Yeyote anayejua kwamba kuna mtoto anayeonewa au kutendewa vibaya hana budi kutoa taarifa kuhusu vitendo hivyo kwa;

- Ustawi wa jamii
- Polisi
- Dawati la jinsia na watoto
- Ofisi za serikali za mtaa
- Timu ya ulinzi na usalama wa mtoto
- Taasisi na Mashirika ya kijamii
- Piga laini ya simu 116 (*bila tozo*)





USTAWI WA MTOTO

# Wajibu wa jumla wa Mtoto

Mtoto ana haki, lakini pia ana wajibu. je, wajibu wa mtoto ni upi?

Pamoja na haki za kulinda ustawi wa mtoto, mtoto atakuwa na wajibu na jukumu la:

(a) Kufanya kazi kwa ajili ya mshikamano wa familia.

(b) Kuwaheshimu wazazi, walezi, wakubwa wake na watu wazima muda wote na atawasaidia pale inapohitajika.

(c) Kuhudumia jamii yake na taifa lake kwa uwezo wake wote kimwili na kiakili kadiri ya umri na uwezo wake.

(d) Kutunza na kuimarisha mshikamano wa jamii na Taifa.

(e) Kutunza na kuimarisha mambo mema katika utamaduni wa jamii na Taifa kwa ujumla katika uhusiano na wanajamii au taifa.

# Utoaji wa haki kwa Watoto

Mahakama maalumu za Watoto hazina budi kuanzishwa ili zishughulike na watoto tu. Mahakama hizi maalumu ziweke mazingira rafiki ili kuhakikisha watoto hawaogopi kwenda Mahakamani na wanapokuwa Mahakamani, watoto wanahaki ya kuwakilishwa na wakili. Vilevile ni lazima waruhusiwe kutoa maoni yao na kueleza yale wanayofahamu kuhusu kilichotokea.

Watoto wanaoshitakiwa kwa kosa la jinai na wanaopelekwa kituo cha polisi wanaweza kuachiwa warudi kwa wazazi wao au wanaweza kupelekwa kwenye nyumba maalumu za kutunza watoto ili kusubiri kesi zao zilizo mahakamani. Watoto hawaruhusiwi kuwekwa gerezani. Utoaji Haki kwa Mtoto wanaopatikana na hatia kwa makosa ya jinai wanaweza kuachiliwa huru kwa sharti la kuonyesha mwenendo mwema, au wanaweza kupelekwa kwenye shule zilizoteuliwa kwa ajili ya utoaji wa Haki kwa Watoto.



# **Tuungane** kukemea na **kupinga mila potofu**





Ulinzi wa mtoto ni jukumu letu sote
Uwe ni baba, mama, ndugu wa familia au jirani.
Pinga ukatili dhidi ya watoto, toa taarifa dhidi ya viashiria hatarishi dhidi ya mtoto wa kike au wa kiume.








www.sawa.or.tz
Morogoro,Tanzania